Africa Journal of Language Studies (AJLS)
Vol. 1 Issue 1 | [November] [2024] | [Page 50] – [Page 63]
Journal homepage: https://ajls.kab.ac.ug
ISSN: 3078-4301

# Kanuni za Mfuatano wa Mofu za Utendeka na Utendana katika Kitenzi cha Kihehe

Na
**Asia Mashaka Akaro**
Taasisi ya Elimu Tanzania
asiagm2015@gmail.com

**Article History:**
**Received:** 15 Jul 2024
**Accepted:** 17 Aug 2024
**Published:** 07 Nov 2024

**Maneno muhimu:**
Mfuatano wa Mofu; Utendeka; Utendana

*This is an open access article under the CC-BY-NC-ND license*

## Ikisiri

Makala haya yanahusu Kanuni za Mfuatano wa Mofu za Utendeka na Utendana zinazojidhihirisha katika vitenzi vya lugha ya Kihehe. Mfuatano wa mofu ikiwa ni namna mofu hizo zinavyojipanga katika kujenga vitenzi kubalifu vya lugha ya Kihehe. Tatizo lililomsukuma mtafiti kufanya utafitihuu ni kukosekana kwa utangamano miongoni mwa wataalamu kama vile: Mpalanzi (2010) kuhusu ruwaza za mfuatano wa utendeka na utendana katika mofu nyambulishi katika lugha ya Kihehe. Data za utafiti zilikusanywa katika wilaya ya Mufindi kwenye kata za Lungemba na Isalavanu katika vijiji vya Lungemba, Munyigumba na Maduma. Miongoni mwa sababu za kuteua eneo hili ni kuwa; kijiografia maeneo haya yako pembezoni mwa miji mikubwa, hivyo, mwingiliano na jamii zingine ni mdogo na hivyo yameihifadhi Kihehe asilia. Pia, haya ndiyo maeneo yanayosadikiwa kuwa ni asili ya lugha ya Kihehe. Zaidi ya hayo, lahaja ya maeneo haya ndiyo lahaja ya mtafiti, hivyo, ilirahisisha mawasiliano wakati wa ukusanyaji data na watoa taarifa. Sampuli ya utafiti ilikuwa ni watu sabini na wawili (72). Utafiti huu uliongozwa na Kanuni Akisi ya Baker (1985) inayosema kuwa mpangilio wa mofu kimofolojia ni lazima ushabihiane na mfuatano wa mofu kisintaksia kutegemea lugha husika. Hii ina maana kuwa iwapo kitenzi fulani kitapitia michakato miwili ya unyambulishaji kama vile, unyambulishaji tendea na tendana, mofu tendea lazima itokee karibu na mofu mzizi kuliko mofimu tendana. Njia za ukusanyaji wa data zilizotumika ni mahojiano na hojaji. Matokeo ya utafiti yanaonesha unyambulishaji tendekaunawakilishwa na mofu //-isik-// katika vitenzi vya silabi moja na mofu //-ik-// kwa vitenzi vyenye silabi zaidi ya moja. Wakati maumbo ya utendana ni mofu //-kwi-// na mofu //-an-//; mofu /-kwi-//inatokea kabla ya mzizi wa kitenzi wakati mofu //-an-// huja baada ya mzizi wa kitenzi. Aidha, kanuni zinazoongoza utokeaji wa maumbo hayo zimeelezwa katika makala haya.

# Principles of Stative and Reciprocal Morph Ordering in Kihehe Verb


## Abstract

This article is about the principles of stative and reciprocal morph ordering in Kihehe verb.Ordering refers to how morphs are arranged in forming acceptable words in Kihehe. The problem inspired this study is mismatch of arguments between by previous scholars Mpalanzi (2010) about stative and reciprocal derivative morphs ordering in Kihehe verbs. The data were collected in Mufundi district at Lungemba and Isalavanu ward through interviews and questionnaires. Speakers of Kihehe language from three villages, namely Lungemba, Munyingumba and Maduma were used.

The reason for selecting these wards and specifically the villages is that the villages are very remote with poor infrastructure which hinders interaction from urban centers. Lack of interaction with urban centers enable villagers to maintain its natural Hehe with less influence from outsiders, unlike other parts. Furthermore, according to oral tradition, this is the area where original Hehe come from. The sample for this study was 72 respondents categorized into two: youth aged between 25 and 35 and elders aged between 50 and 80. The study was guided by Mirror Principle as founded by Baker (1985) which contends that morphological ordering known via the morph order must match the syntax and vice versa. It further states that if a verb undergoes two derivatives; for example, applicative and reciprocal, then applicative derivatives should appear closer to the verb root than the reciprocal. The study results indicate that stative morphs is //-isik-// in monosyllabic verbs and morphs //-ik-// for polysyllabic verbs. The reciprocal morphs are //-kwi-// and //-an-//. Morph //-kwi-// appear before root verbs and morphs //-an-// comes after the root verbs. Principle governing the ordering has been indicated.


**Keywords: Stative, Reciprocal, Morph Ordering**

## 1.0 Utangulizi

Lugha ya Kihehe ni miongoni mwa lugha za Kibantu inayopatikana katika kundi la G.60, ikijumuishwa na lugha za Kikinga na Kibena (Guthrie, 1948). Tofauti na Guthrie (keshatajwa) uainishaji uliofanywa na Nurse (2008) umeiweka lugha ya Kihehe kama lugha ya Kibantu ya lugha za kundi la G.62 iliyopo katika kundi lijulikanalo kama kundi la Kibena-Kikinga cha Niger. Licha ya wataalamu hawa wawili kuiweka lugha ya Kihehe katika makundi tofauti, lakini wote wanaona Kihehe kina uhusiano namakundi ya lugha zingine zinazopatikana ukanda wa nyanda za juu kusini. Makundi mengine ni pamoja na Kisangu (G.61), Kibena (G.63), Kipangwa (G.64), Kikinga (G.65), Kiwanji (G.66) na Kikisi (G.67). Uhusiano wake upo katika vipengele vya msamiati, kanuni za kifonolojia na katika baadhi ya sifa za kimofolojia kama vile: maumbo ya umoja na wingi, njeo, nafsi na ukanushi. Uchunguziuliofanywa kuhusu kanuni za mfuatano wa mofu katika vitenzi vya lugha hizi hakuna utangamano miongoni mwa wataalamu kama vile Mpalanzi (2010) na Gawasike (2011). Tofauti za kimtangamano zipo katika aina ya idadi ya mofu zinazoweza kufuatana na pamoja na nafasi inayokaliwa na aina fulani katika safu ulalo wake. Utafiti huu ulilenga kubainisha mfuatano wa mofu za utendeka na utendana katika Kihehe kisha kueleza kanuni zinazoukilia mfuatano huo.

Aidha, kuhusu unyambulishaji wa vitenzi katika lugha za Kibantu, wanaisimu wametofautiana pia kuhusu aina na idadi ya minyambuliko hiyo kama ifuatavyo: Doke (1943), amebainisha

minyambuliko kumi na saba (17), Ashton (1944) na Jonsson (1949), wamebainisha minyambuliko kumi na nne (14). Massamba na wenzake (2012) wamebainisha aina sita tu (06). Mjadala wa tofauti na vigezo walivyotumia katika kupata aina hizo viko nje ya utafiti huu. Kwa kuwa minyambuliko, mitano ifuatayo: usababishi, utendea, utendana, utendeka na utendwa imebainishwa na wataalamu wote tuliowataja hapo juu; na kwa kuwa Kihehe nacho ni miongoni mwa lugha za Kibantu (Guthrie 1948), hivyo kazi hii inachunguza minyambuliko na mifuatano ya mofimu nyambulishi zinazohusu aina mbili za minyambuliko utendana na utendeka kwa kuwa inaelekea kuafikiana na wataalamu wengi wa isimu kuwa inapatikana katika sarufi ya lugha nyingi za Kibantu, Kihehe kikiwa ni miongoni mwake.


## 1.1 Sauti za Lugha ya Kihehe

Tafiti anuwai zilizofanywa kuhusu lugha ya Kihehe zinaonesha kuwa ina jumla ya fonimu ishirini na tisa (29) ambapo Irabu zipo kumi (10) na konsonanti kumi na tisa (19). Aidha, licha ya Schröder (2008) kudai kuwa lugha za Kibantu zina irabu saba lakini lugha ya Kihehe ina zaidi ya irabu hizo saba kwa sababu karibu katika kila aina ya irabu kuna irabu ndefu na irabu fupi. Ukizihesabu kwa pamoja zinazidi idadi hiyo inayoelezwa na Schröder (keshatajwa). Kwa kuwa lugha ya Kihehe ni lugha yenye irabu ndefu na fupi, idadi yake ni kumi (10). Kielelezo namba 1.1 kinadhihirisha hali hiyo.

### 1.1.1 Irabu za Kihehe

Kama tulivyodokeza hapo awali katika §1:1 hapo juu lugha ya Kihehe ina irabu zaidi ya kumi (10) ambazo ni fupi na ndefu. Aidha, kama ilivyo kwa baadhi ya lugha ulimwenguni kadhalika irabu za lugha ya Kihehe hubainishwa kwa kuzingatia mwinuko wa ulimi (juu, kati na chini), mahali/sehemu ya ulimi (mbele, kati na nyuma) na umbo la midomo (viringe, siviringe). Hoja hii inashadidiwa na mifano katika kielelezo kifuatacho:

**Kielelezo Na.1.1: Kuonesha Irabu za Lugha ya Kihehe**




**Chanzo:** Data ya Uwandani

Kielelezo namba 1.1 kinaonesha mkao wa irabu za lugha ya Kihehe. Aidha, kielelezo hicho kinaonesha kuwa kila irabu ina urefu na ufupi na idadi yake jumla zinafika kumi. Lugha ya Kihehe ina irabu nne za juu: (i/i: u/u:), irabu nne za kati (e/e:, o/o:) na irabu mbili za chini (a/, a:). Jumla yake inafanya irabu 10 na siyo saba kama Schröder (keshatajwa) anavyodai. Vilevile, kielelezo hiki kinadokeza kuwa, lugha ya Kihehe ina irabu nne (i/i: e/e:) ambazo zinatamkwa ulimi ukiwa mbele, irabu mbili (a/, a:) hutamkwa ulimi ukiwa katikati na irabu nne (u/u:, o/o:) hutamkwa ulimi ukiwa

nyuma. Aidha, irabu tano (u/u:, o/o:, a) hutamkwa midomo ikiwa viringe na irabu tano (e/e:, i/i:, a:) hutamkwa midomo ikiwa siviringe. Kwa hivyo, muundo huo wa irabu kwa maana ya kuwako kwa irabu ndefu na fupi katika lugha ya Kihehe, unaweza kuathiri mfuatano wa mofu zinazouunda maneno ya lugha hii. Kwa sababu utamkaji wa maneno yenye irabu fupi ni tofauti na utamkaji wa maneno yenye irabu ndefu, Massamba (2011).

### 1.1.2 Konsonanti za Kihehe

Lugha ya Kihehe ina jumla ya konsonanti kumi na tisa (19) ambazo hubainishwa kwa jinsi na mahali pa matamshi kama inavyodhihirishwa katika jedwali lifuatalo:

### Jedwali Na. 1. 1: Konsonanti za Lugha ya Kihehe

| **Jinsi ya Matamshi** | **Mahali pa Matamshi** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Midomo | midomo-meno | Ufizi | kaakaa gumu | kaakaa laini | Koromeo |
| Vipasuo | p b | | t d | | k g | |
| Vikwamizi | | | f | č | | |
| Vizuio-kwamizi | | f v | s | | | h |
| Nazali | m | | n | ɳ | ŋ | |
| Vitambaza | | | l | | | |
| Viyeyusho | w | | | y | | |

**Chanzo:** Data ya Uwandani

Kama jedwali na. 1.1 linavyoonesha, lugha ya Kihehe ina jumla ya konsonanti kumi na tisa (19). Katika maandiko yaliyotangulia kama vile, Mpalanzi (2010) anadai kuwa, lugha hii ina konsonanti [β], [γ], [š] na [r]. Hata hivyo, hoja hiyo inasailika ukizingatia matamshi ya watoa taarifa wa Kihehe. Watoa taarifa ambao ni Wahehe hutamka fonimu hizo kama ifuatavyo: sauti [r] hutamkwa [l]; kwa mfano neno furaha hutamkwa fulaha; sauti gh hutamkwa g; kwa mfano neno, ghali hutamkwa gali; sauti [š] hutamkwa [s], kwa mfano, neno shuka hutamkwa suka na neno thumuni hutamkwa sumuni. Kutokana na mazingira hayo ya utamkaji wa fonimu zilizobainishwa na Mpalanzi (2010) kwamba ni sehemu ya konsonanti za lugha ya Kihehe inatia mashaka. Kihehe kinaelekea kutokuwana sauti hizo, yaani [β], [γ], [š] na [r].

## Kiunzi cha Kinadharia

Makala haya yaliongozwa na Kanuni Akisi ya Baker (1985 na 2002). Kanuni hii inaoeleza kuwa upo uhusiano wa karibu kati ya mofolojia na sintaksia. Kwamba, *unyambulishaji kimofolojia*[89] sharti uakisi unyambulishaji wa kisintaksia. Tunaelewa unyambulishaji unahusu kuongeza viambishi (mofu) baada ya mzizi wa neno. Unyambulishaji huo huleta athari za kisintasia kwa kuongeza dhima, kupunguza dhima au kudhibiti dhima (Wesana-Chomi, 2017). Kwamba hiyo michakato ya kimofolojia inaweza kuathiri mpangilio wa maneno katika sintasia; kwa ama kuongeza au kupunguza washiriki katika tungo. Kwa mujibu wa Baker (2002), sintaksia inatenda kazi katika sehemu mbili; mofu na neno. Kipashio cha msingi cha uchanganuzi wa kisitntaksia ni neno na kipashio cha msingi cha uchanganuzi wa kimofolojia ni mofu. Mchakato unaofanyika

katika neno huathiri muundo wa sentensi. Anafafanua zaidi kuwa, maneno changamani huundwa na kanuni za kisintaksia hasa, mjongeo wa neno kuu kwa kugubika mzizi leksia katika mofu.

[89]Neno *"vialamishi kimofolojia"* tumetumia kutoka katika neno la Kiingereza *"Morphological Marker".*

Kanuni hii inaeleza zaidi kwamba, elementi zote zinazohusu mofolojia na sintaksia huathiriana katika mpangilio wa vijenzi vyake. Hapa kinachoangaliwa ni athari za unyambulishaji wa vitenzi kisintaksia. Kanuni Akisi ya Baker inaona kuwa unyambulishaji kimofolojia unaakisi unyambulishaji sintaksia na kinyume chake. Kwa maana hii kwamba, ikiwa muundo wa kimofolojia wa neno changamani umetokana na mjongeo wa mzizi leksia katika maneno ambao mofu hizo zimeambikwa, basi Kanuni Akisi hufuatia moja kwa moja. Kama anavyoeleza Baker kuwa mfuatano wa mofu katika neno changamani unaakisi uambatizi asilia kisintaksia wa maneno ambayo yanashabihiana na mofu hizo (Baker 2002: 326).

Kuibuka kwa Kanuni Akisi hii kulitokana na kusaili mtazamo wa sarufi zalishi uliojikita zaidi katika kuangalia dhima ya virai nomino na dhima za kidhamira na kupuuza vialamishi kimofolojia kama vile urejeshi, ambavyo vikiachwa tu vinaleta mvunjiko wa muundo wa sarufi. Pili, kikanuni, upo uwezekano mkubwa wa kuunda utendwa, kwa kuambika mofu za utendwa katika nomino ambao ni sawa na uwezekano uliopo wa kuundwa umbo tendwa kwa kuambika mofu tendwa katika vitenzi. Baker (keshatajwa) anafafanua kuwa unyambulishaji sintaksia unaukilia mfuatano wa mofu si tu katika lugha za Kibantu, Kihehe kikiwa miongoni mwake bali pia kiisimu kwa ujumla. Mpangilio wa kimofolojia hubainishwa na mfuatano wa mofu ambao ni lazima ushabihiane na mfuatano wa mofu kisintaksia wa lugha husika. Kwa mfano, mpangilio wa mofu za utendeka na utendana katika lugha ya Kihehe sharti ziafikiane na wazungumzaji wazawa wa lugha hiyo kwenye tungo zao. Hii ina maana kuwa iwapo kitenzi kitapitia michakato miwili ya unyambulishaji, tuseme kwa mfano, unyambulishaji tendea na tendana, mofu tendea lazima zitokee karibu na mofu mzizi kuliko mofu tendana. Manova na Aronoff (2010), wanabainisha sababu kuu mbili zinazosababisha hali hii. Sababu hizi ni utokeaji wa mofu unaotawaliwa na kanuni na utokeaji wa mofu usiotawaliwa na kanuni. Tunatoa ufafanuzi wa sababu hizo katika aya inayofuata.

Kwanza ni utokeaji wa mofu unaotawaliwa na kanuni. Hii ni sababu inayohusisha kanuni rasmi za kisarufi zinazohusisha uzingativu wa umbo na maana. Umbo na maana vimejiegemeza katika masuala yahusuyo kanuni za kifonolojia, kanuni za kimofolojia, kanuni za kisintaksia na kanuni za kisemantiki. Kwa ujumla hii inahusisha michakato mbalimbali ya kimofofonolojia na michakato ya kimofosintaksia. Aidha, Massamba (2016) anazifafanua dhana hizi mbili kama ifuatavyo: mofofolonolojia ni taaluma ya isimu inayohusu uchanganuzi na uainishaji wa vipengele vya kifonolojia vinavyoathiri maumbo ya mofimu au vipengele vya kisarufi vinavyoathiri maumbo ya fonimu. Mofosintaksia kwa upande wake ni taaluma ya isimu inayoshughulikia uchambuzi, uchanganuzi na uainishaji wa uhusiano uliopo baina ya mofolojia na sitantaksia. Kwa upande mwingine utokeaji wa mofu usiofungwa na kanuni (yaani utokeaji wa mofu kinasibu) unahusu masuala ya uolezi na unasibu. Makala haya yamezingatia utokeaji wa mofu unaotawaliwa na kanuni za kimofolojia. Baker (1985), katika mifano yake kama alivyonukuliwa na Mcpherson (2008:107) alitumia lugha ya Kijapani na Kibemba kama ioneshwavyo katika mfano wa kwanza hapa chini. Aidha, mifano hiyo inaonesha zaidi kuwa alitumia unyambulishaji fanyizi na unyambulishaji

tendwa.

Kwa mfano:

1. (a) tabe-sase-rare-ta
eat-CAUS-PASS-PAST
'was made to eat'

(b) Mwape-aa-man-esh-wa Mutumba na ine
Mwape 3SGS-see-CAUS-PASS Mutumba by me
'Mwape was made to see Mutumba by me' (Baker 1985:396)

Katika mifano hii kitenzi 'kula' kwanza kinapitia mchakato wa unyambulishaji fanyizi (usababishi) kisha unyambulishaji utendwa. Aidha, mofu za usababishi zimetokea karibu na mzizi kuliko mofu za utendwa. Katika mfano wa pili, unyambulishaji tendea na unyambulishaji tendana ni kama ifuatavyo:

| 2. | | | |
|---|---|---|---|
| | a) pika | pikiana | pik-i- an-a |
| | b) soma | someana | som-e-an-a |
| | c) funga | fungiana | fung-i-an-a |
| | d) sema | semeana | sem-e-an-a |

Mifano ya data hiyo kwa lugha ya Kiswahili inaonesha kuwa kimfuatano, mofu nyambulishi ya utendea huwa karibu na mzizi na kufuatiwa na mofu nyambulishi ya utendana. Aidha, kwa kutumia Kanuni Akisi, tunaweza kuchunguza mifuatano ya mofu nyambulishi ya utendeka na utendana katika lugha ya Kihehe. Hivyo, katika kuchunguza mfuatano wa mofu nyambulishi wa vitenzi vya Kihehe tutatumia Kanuni Akisi, kwa sababu kanuni hii inatuwezesha kueleza mifuatano ya mofu nyambulishi katika lugha hii hasa utendeka na utendana.

## Methodolojia za Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika vijiji vya Lungemba, Munyigumba na Maduma vilivyopo wilaya ya Mfindi katika mkoa wa Iringa. Maeneo hayo yalichaguliwa kwa sababu yapo pembezoni mwa mji, hali inayosababisha uhafifu katika kuathiriana na lugha nyinginezo kutokana na uchechefu wa muwasala wa jamii hii na jamii zingine nje ya mazingira haya. Halikadhalika, mapokeo simulizi ya kihistoria yanaonesha kuwa, haya ndiyo maeneo yanasadikiwa kuwa ni miongoni mwa sehemu ambazo ni chimbuko la lugha ya Kihehe. Pia, Kihehe kizungumzwacho maeneo hayo ni lahaja ya mtafitiwa, hivyo, ilirahisisha mawasiliano wakati wa ukusanyaji data.

Ama kuhusu njia za ukusanyaji wa data, utafiti ulikusanya data kwa njia mbili; hojaji na mahojiano. Vijana walijaza hojaji na wazee walishiriki katika mahojiano na mtafiti. Sampuli ya watoa taarifa katika utafiti huu ilikuwa ni watu sabini na wawili (72) kutoka jamii ya Wahehe waliogawanyika katika makundi makuu matatu: jinsia, elimu na umri. Kwa upande wa umri, kulikuwa na vijana wa umri kati ya miaka 20-30 (idadi watu 33) na wazee wa umri kati ya miaka 50-80 (idadai watu 39) walichaguliwa. Kundi la vijana hawa walijaza hojaji na wazee walishiriki katika mahojiano. Kwa upande wa elimu, kundi la wazee ni wale ambao hawakusoma kabisa, lakini wanakielewa vyema Kihehe, hivyo walishiriki kwa njia ya mahojiano. Aidha, kwa makundi yote mawili, kulikuwa jinsi ya kiume na ya kike. Mgawanyo wa sampuli ni kama jedwali nambari 1.2 linavyoonesha:

**Jedwali Na. 1.2: Mgawanyo wa Sampuli ya Utafiti**

| Watoa taarifa | Lungemba | | Munyigumba | | Maduma | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ME | KE | ME | KE | ME | KE | **Jumla** |
| Vijana umri wa miaka 25- 35 | 5 | 5 | 5 | 6 | 6 | 6 | **33** |
| Wazee Umri wa miaka 50-80 | 7 | 7 | 6 | 7 | 6 | 6 | **39** |
| **Jumla** | **12** | **12** | **11** | **13** | **12** | **12** | **72** |

**Chanzo:** Utafiti

Sampuli ya utafiti huu ilipatikana kwa njia ya usampulishaji tajwa. Mtafiti alifika katika vijiji vilivyotumika kupata data, na kufikia kwa Mwenyekiti wa Serikali ya kijiji; kisha alimwomba mwenyekiti amtajie kijana ambaye amemaliza kidato cha sita kijijini hapo. Kisha baada ya kumpata kijana wa kwanza, mtafiti alikutana na kijana huyu, alimwomba kijana huyo amtajie vijana wengine ambao wapo kijijini hapa na wamehitimu kidato cha sita. Lengo likiwa kupata vijana wa Kihehe waliofika kidato cha sita. Baada ya kupata idadi husika kwa kila kijiji; mtafiti aliwapatia vijana hawa hojaji na kuwaomba wazijaze.

Walipewa muda wa juma moja kukamilisha, baada hapo mtafiti alizikusanya hizo hojaji. Hojaji ilikuwa na vitenzi sabini na mbili (72) vilivyokuwa vimeandikwa kwa Kiswahili. Vitenzi hivyo vilikuwa katika umbo la unyambulishi tendeka na tendana; watoa taarifa walihitaji kuviandike vitenzi hivi kwa lugha ya Kihehe. Kila Kijiji kilikuwa na hojaji yenye vitenzi vya maumbo haya kumi na tano (15). Njia hii iliteuliwa kwa sababu inampa uhuru mtoa taarifa kujaza taarifa zake akiwa katika hali ya usiri na utulivu mkubwa. Aidha, wakati wa uchanganuzi wa data, mtafiti alizingatia suala la athari za kitahajia zinazoweza kuwa zimekosewa na mtoa taarifa, kisha kuweka sawa.

Kwa upande wa sampuli ya wazee wa umri wa miaka 50-80 yalifanyika mahojiano na mtafiti. Mahojiano ni majibizano au mazungumzo ya ana kwa ana (au ya simu, kidijiti/barua pepe)kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu suala fulani la kiutafiti lililoainishwa (Kothari, 2009). Aidha, Mligo (2012) anaeleza kuwa mahojiano hutumika katika maeneo halisi waishio watu. Katika utafiti huu, mahojiano yalifanyika kati ya mtafiti na mtu mmoja mmoja. Kwa sababu mtafiti alilenga kuchunguza namna mtu mmoja mmoja anavyotumia lugha ya Kihehe katika mawasiliano ya kawaida. Mazungumzo baina ya mtafiti na mtoa taarifa mmoja mmoja yalifanywa ulinganifu na majibu ya wengine, kisha kufanya hitimisho kuhusu muundo wa maneno lugha ya Kihehe. Watoa taarifa 39 walijumuishwa kutoka kwenye vijiji vitatu ambapo kila kijiji alihojiana na watu 13 wa jinsi tofauti. Mahojiano haya kimsingi yalihusiana na orodha ya msamiati ambao vijana walishughulikia katika hojaji. Lengo ilikuwa ni kuoanisha data ya vijana na wazee, na kisha kuhitimisha kuhusiana na mpangilio wa vijenzi vya maneno ya lugha ya Kihehe.

## Uchanganuzi wa Data

Makala haya yanahusu kanuni za mfuatano wa mofu nyambulishi za utendeka na utendana katika vitenzi vya lugha ya Kihehe. Katika kuwasilisha taarifa za utafiti huu, sehemu hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo:

Unyambulishaji wa vitenzi vya Kihehe kwa ujumla na uyumbulishaji wa utendeka na utendana

katika Kihehe. Maelezo ya mfuatano wa mofu nyambulishi za utendeka na utendana katika lugha hii yamebainishwa. Mwisho, kwa kuongozwa na Kanuni Akisi ya Baker (1985) tumeonesha kanuni zinazotawala huo mfauatano.

## Unyambulishaji wa Utendeka na Utendana wa Vitenzi vya Kihehe

Utafiti huu haukulenga kuchunguza unyambulishaji wa vitenzi katika lugha ya Kihehe ila kubainisha mfuatano wa mofu na kanuni zinazotawala mfuatano huo. Hata hivyo, ni muhimu kuonesha maumbo ya unyambulishi wa mofu husika kwani ndiyo yanayoelekea kuchunguzwa katika utafiti huu. Katika utafiti huu, dhana ya unyambulishaji tunaizingatia kama ilivyoelezwa na Gawasike (2012) kuwa unyambulishaji ni upachikaji wa viambishi nyambulishi baada ya mzizi wa kitenzi. Aidha, licha ya kuwa kuna aina mbalimbali za unyambulishaji, utafiti huu umeonesha aina mbili tu ambazo ni unyambulishaji tendeka na tendana. Matokeo yanaonesha kuwa, mofu ya utendeka na utendana hupachikwa mara tu baada ya mzizi wa kitenzi kama jedwali Na. 1.3 hapo chini linavyoonesha. Kwa mantiki hii, lugha ya Kihehe ni miongoni mwa lugha za Kibantu ambazokwazo mofu nyambulishi huweza kupachikwa baada ya mzizi wa kitenzi.

### Jedwali Na. 1.3: Unyambulishaji Tendeka na Tendana wa Vitenzi vya Lugha ya Kihehe //-ik-// na Tendana //-kwi-/ -an-//

| Na. | Utenda | Maana | Utendeka | Maana | Utendana | Maana |
|---|---|---|---|---|---|---|
| i. | -ly-a | la | ly-isik-a | lika | kwi-ly-a | *kulana |
| ii. | tov-a | piga | tov-ek-a | pigika | kwi-tov-a | Pigana |
| iii. | long-a | sema | long-ek-a | semeka | long-an-a | Semana |
| iv. | suk-a | omba | suk-ik-a | ombeka | suk-ana | Ombana |

**Chanzo:** Utafiti

Data katika Jedwali Na 1.3 zinaonesha unyambulishaji maumbo ya mofu nyambulishi katika lugha ya Kihehe. Mofu za utendeka ni (//-isik-//; na //-ek-//) na ambazo hutokea baada ya mzizi wa kitenzi wakati mofu za utendana ni (//-an-//). Aidha, alama ya nyota katika safu wima ya mwisho kulia inadokeza maana isiyokubalifu katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, katika lugha ya Kihehe maana hiyo inakubalika hasa kwa kuzingatia muktadha wa matumizi. Kiutamaduni, mtu mmoja akiwa anaroga watoto au familia nyingine na kuwaua kiushirikina; na familia ya pili ikafanya malipizi ya aina hiyo hiyo. Basi watu hawa, *wanakulana watoto wao. Kadhalika, vijana wanaojihusisha na masuala ya kigono, huweza kutumia kwama mvula fulani, tusema X *anakulana na msichana fulani tuseme Y; kwa maana kwamba wanafanya ngono. Katika mawasiliano ya kawaida na ambayo ni rasmi, si kawaida kutumia kitenzi hicho katika hali ya kutendana.


### Unyambulishaji wa Utendeka katika Vitenzi vya Silabi Moja

Kwa mujibu wa Mgullu (1999), vitenzi vyenye silabi moja ni aina ya vitenzi ambavyo mzizi wake umejengwa au umeundwa na silabi moja tu. Mgullu (keshatajwa) anaeleza zaidi kuwa, katika lugha ya Kiswahili vitenzi hivi huambatanishwa na kiambishi kiso ukomo (ku-) katika utenda ili kuleta maana. Halikadhalika katika lugha ya Kihehe vitenzi vya silabi moja huwa na ruwaza ya kuambatana na mofu //ku-// ili kuleta uamilifu wa kimaana katika utenda.

Kiambishi //ku-// ni kijenzi muhimu katika vitenzi vya silabi moja. Uchunguzi uliofanywa na utafiti huu kuhusu unyambulishaji, unaonesha matokeo kama katika mifano ifuatayo:

| 01. | Utenda | Maana | Utendeka | Maana |
|---|---|---|---|---|
| (i) | -ly-a | la | ly-isik-a | lika |
| (ii) | -nyu-a | nywa | nyu-esek-a | nyweka |
| (iii) | -fw-a | fa | fw-isik-a | *fika |
| (iv) | -sa | ja | *s-ik-a | *jika |

Kama data kutoka kwenye mfano wa 1 hapo juu inavyoonesha unyambulishaji wa utendeka wa vitenzi vya silabi moja katika Kihehe unawakilishwa na mofu //-isik-// ambayo ina alomofumbili, {-isik-} na {-esek-}. Alama ( ) inadokeza kuwa tafsiri sisisi iliyofanyika katika lugha ya Kiswahili haikubaliki kimaana katika matumizi ya kawaida ya lugha hiyo. Kwa mfano, kitenzi *kulana ingawa kinaweza kuashiria maana fulani, lakini maana hiyo ni hasi na ni ya kimuktadha fulani pekee. Miktadha hiyo inayokubali maana hii inaweza kuwa ni kwa vijana wenye rika sawa au ni kwa wazee wanaoshiriki ulozi. Hivyo, utokeaji wa alomofu za mofu tendeka katika vitenzi hivyo unaweza kurasmishwa kikanuni kama inavyooneshwa katika:

01.



Kanuni hii kutoka kwenye mfano wa data za ya 1 ya vitenzi vya silabi moja inafasiliwa kama mofu {-isik-} inajitokeza kama mofu katika mazingira ambamo mzizi wa kitenzi unaishia na konsonanti kama vile: -ly- na -fw- ilhali alomofu {-esek-} inajitokeza ikiwa mzizi wa kitenzi unaishia na irabu (-i- na -u-) kwa mfano: -nyu- na -nyi-.

## Unyambulishaji wa Utendana wa Vitenzi vya Silabi Moja katika Kihehe

Unyambulishaji wa utendana unahusu wahusika wawili au zaidi katika tungo kutendeana jambo kwa kiasi sawa. Ashton (1944) anaeleza kuwa utendana ni hali ya kitenzi kinachohusisha pande mbili katika utendaji wa jambo katika mizania iliyo sawa sawa. Kama tulivyoeleza hapo awali, utendaji huu ni kiasi au kiwango sawa. Katika lugha ya Kihehe umbo au mofu ya utendana ni //-kwi-//. Aidha, vitenzi vya silabi moja vilivyo katika hali ya utendana hufungamana zaidi na maana ya kinahau. Maana ya kinahau ni aina ya maana ambayo hupatikana kwa kurejelea muktadha mahususi ambamo umbo hilo limetumika. Maumbo haya ni kama inavyooneshwa katika mfano 2 hapa chini:

| 02. | **Utenda** | **Fasiri ya Kiswahili** | **Utendana** | **Maana** |
|---|---|---|---|---|
| (i) | -lya | la | kwi-ly-a | *lana |
| (ii) | -nyua | nywa | kwi-nyu-a | nywana |
| (iii) | -fwa | fa | *kwi-fw- | *fana |
| (iv) | -sa | ja | *kwi-s-a | *jana |

**Chanzo:** Utafiti

Kama mifano ya data kutoka mfano wa 2 hapo juu inavyoonesha; mofu ya utendana katika vitenzi vya silabi moja inawakilishwa na umbo //-kwi-// ambalo hutokea mwanzoni mwa mzizi wa kitenzi.

Tofauti kabisa na lugha ya Kiswahili, umbo la utendana huja baada ya mzizi wa neno; lugha ya Kihehe inaleta ruwaza tofauti. Alama ya nyota (*) katika kwenye data ya mfano wa 2 hapo juu inaashiria kuwa neno husika kimofolojia halikubaliki katika lugha ya Kihehe na Kiswahili kadhalika. Aidha, mifano hii inaonesha zaidi kuwa katika lugha ya Kihehe vitenzi hivi hubeba maana za kinahau. Kwa mfano, vitenzi kwi-ly-a na kwi- nyu-a havina maana halisi ya kulana ama kunywana bali maana zake hutokana na muktadha kilimotumika au jamii. Kwa mfano katika jamii ya Wahehe ni jambo la kawaida kusikia, mtu X (labda Lumato) amekula watoto wa mzee fulani (Tuseme Madumulla au kusikia mzee Madumulla anakula watoto wa ndugu Lumato). Aidha, ni kawaida kusikia familia X (labda Lumato) wananyweana pombe na familia Y (tuseme Madumulla). Katika kitenzi nyweana hapo, kinaashirikiana kushirikiana katika kutumia pombe ambayo aghalabu hutayarishwa na familia mojawapo kati ya hizo mbili zilizorejelewa hapo kwenye maelezo. Kiutendana Lumato na Madumulla wanakulana watoto wao. Maana ya kauli hiyo na ukubalifu wake unaukiliwa na masuala ya kimuktadha wa kijamii. Hata hivyo, sio jambo la kawaida kuwa na utendana wa kitenzi kula katika lugha ya Kiswahili.

## Unyambulishaji wa Utendeka na Utendana katika Kitenzi vya zaidi ya Silabi Moja

Kama ilivyoelezwa kwingineko katika makala haya ni kuwa, lengo la utafiti lilikuwa ni kubainisha mfuatano wa mofu za mnyambuliko za utendeka na utendana katika vitenzi vya lugha ya Kihehe. Katika sehemu hii tunabainisha mofu nyambulishi katika vitenzi vyenye silabi zaidi ya moja.

## Unyambulishaji wa Utendeka katika Vitenzi vyenye Silabi zaidi ya Moja

Uchunguzi wa utafiti huu unaonesha kuwa, mofu za utendeka kwa vitenzi vyenye silabi zaidi ya moja ni //-ik-// ambayo ina alomofu mbili, yaani: {-ik-} na {-ek-}. Aidha, utokeaji wa maumbo ya utendeka ni tabirifu, kwani mazingira yake yanaukiliwa na umbo la mzizi wa kitenzi. Kwa mfano katika 3 hapa chini inaonesha hali hiyo:

| 03. | **Utenda** | **Tafsiri ya Kiswahili** | **Utendeka** | **Maana** |
|---|---|---|---|---|
| | (i)dakul-a | tafuna | dakul-ik-a | tafunika |
| | (ii)bet-a | vuna | bet-ek-a | vunika |
| | (iii)kin-a | cheza | kin-ik-a | chezeka |
| | (iv)tov-a | piga | tov-ek-a | pigika |

## Chanzo: Utafiti

Data katika 03 inaonesha kwamba, mofu ya utendeka katika Kihehe ni //-ik-// ambayo ina alomofu mbili: {-ik-} na {-ek-}. Alomofu hizo hutokea katika mazingira ambayo yanatabirika. Utabirifu huu unaelekea kutokea pia katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, alomofu {-ik-} hutokea kwenye vitenzi ambavyo mizizi yake inaishia irabu (-a-, -i- na -u-) wakati alomofu {-ek-} hutokea kwenye vitenzi ambavyo mzizi ina irabu (-e- na -o-). Maelezo haya yanaweza kuundiwa kanuni kama ifuatavyo:

02. //-ik-// ⟶ - ik- Mz
-a-
-i-
-u-

→ -ek- } Mz
-e-
-o-

## Unyambulishaji wa Utendana katika Vitenzi vyenye Silabi zaidi ya Moja

Lugha ya Kihehe; tofauti na lugha ya Kiswahili inaonesha kuwa ina maumbo mawili yanayowakilisha mofu ya utendana. Kiswahili kina umbo moja pekee linaloashiria utendana. Kati ya watoa taarifa sabini na wawili (72) walioshiriki katika utafiti huu, watoa taarifa sitini na tatu (63) wanaonesha kuwa mofu ya utendana katika Kihehe ni //-kwi-// na watoa taarifa tisa (9) wanaonesha kuwa umbo la utendana katika Kihehe ni //-an-//. Katika mahojiano na wazee wenye umri wa miaka 50-80 kila walipokutana na umbo la utendana katika Kiswahili, walipotakiwa kuliweka katika lugha ya Kihihe, mofu //-kwi- ndiyo iliyopachikwa katika data hiyo. Aidha, kundi la vijana kwa upande mwingine kulikuwa na matokeo mchanganyiko. Kati ya watoa taarifa 33, watoa taarifa ishirini na wa nne (24) walibainisha umbo //-kwi-.// kama umbo la utendana katika vitenzi vya Kiswahili. Ni watoa taarifa tisa (9) pekee kutoka kundi la vijana waliobainisha mofu //-na-// kuwa ndilo linalowakilisha utendana katika vitenzi vya Kihehe. Data katika jedwali Na. 1.3 linadhihirisha hali hiyo.

### Jedwali Na. 1.3: Maumbo ya Utendana katika Vitenzi vya Kihehe

| Na. | Utenda | Maana | Utendana | Maana |
|---|---|---|---|---|
| i. | dag-a | fukuza | kwi-dag-a | fukuzana |
| ii. | deny-a | vunja | kwi-deny-a | vunjana |
| iii. | gav-a | gawa | gav-an-a | gawana |
| iv. | long-a | sema | long-an-a | semana |

**Chanzo:** Utafiti wa Uwandani

Kama jedwali namba1.3 linavyoonesha, Kihehe kinaruhusu kupachika umbo la utendana kabla ya mzizi wa kitenzi. Kwa mfano, data kutoka kwenye jedwali katika (i) na (ii) inadhihirisha hali hiyo. Kama tulivyokwishadokeza hapo juu, hiki ni kitu cha kipekee. Lugha nyingi za Kibantu Kiswahili kikiwa miongoni mwake, maumbo ya unyambulishi (au vinyambuo) ikiwa ni pamoja na unyambulishi wa utendana hutokea baada ya mzizi wa neno. Aidha, mahojiano na wazee wazawa wa lugha ya Kihehe kwa kiasi kikubwa walielekea kutokubaliana na umbo nyambulishi //-na-// ambalo linatokea baada ya kitenzi. Yumkini utafiti mpana na wa kina kwa maana ya ukubwa wa data kuhusu jambo hili unahitajika kufanyika ili kuona hali halisi ikoje katika suala la unyambulishaji wa vitenzi vya Kihehe hasa katika mofu ya utendana. Kadhalika, upanuaji wa sampuli ya utafiti, kwa maana ya washiriki inaweza kusaidia kutoa hitimisho linalotoa mwelekeo halisi juu ya nafasi ya utokeaji wa umbo nyambulishi la mofu ya utendana //-na-//Aidha, data katika jedwali inaonesha zaidi kuwa, mofu nyambulishi ya utendana //-kwi-// kwa vitenzi vyenye silabi zaidi ya moja katika lugha ya Kihehe ni: {-kwi-} na {-an-}; ambapo mofu //-kwi-// inajitokeza mwanzoni mwa mzizi wa kitenzi wakati mofu //-an-// inatokea baada ya mzizi kitenzi. Utokeaji wa mofimu hizo unaweza kurasmishwa kikanuni kama katika 03.

03. //-kwi-// ⟶ -kw- | # ——

⟶ {-an- } | # —— kwingineko

Kanuni ya 3 hapo juu inafasiriwa kwamba, mofu {-kwi-} hutokea katika mazingira ya mwanzoni mwa mzizi wa kitenzi na mofu {-an-} hutokea katika mazingira mengineyo. Aidha, utokeaji wa mofu //-kwi-// ni tabirifu wakati utokeaji wa mofu /-na-// si tabirifu.

## Mfuatano wa Mofu za Utendeka na Utendana katika Vitenzi vya Lugha ya Kihehe

Katika sehemu zilizotangulia tumebainisha unyambulishaji wa vitenzi vya Kihehe, katika sehemu hii tunaonesha mfuatano wa mofu nyambulishi za utendeka na utendana katika Kihehe. Uchunguzi uliofanywa na utafiti huu umebaini mifuatano ifuatayo:

### Mfuatano wa Utendeka +Tendana (//-isik- + -kwi-//)

Kutokana na data ya uwandani imebainika kuwa mfuatano wa mofu nyambulishi za utendeka na utendana kwa vitenzi vya silabi moja haujitokezi kabisa. Watoa taarifa walibainisha kwamba katika lugha yao hakuna ruwaza ya mfuatano huo. Hivyo, kutokana na makala haya, tunahitimisha kuwa mfuatano wa mofu nyambulishi za utendeka – tendana katika vitenzi vya silabi moja haupo. Aidha, kwa kuzingatia Kanuni Akisi ya Baker (1985) inayoeleza kuwa unyambulishi kisintaksia lazima uakisi mofolojia ya lugha husika, lugha ya Kihehe hata kitenzi kikiwekwa katika muktadha wa matumizi ya sentensi, mfuatano wa utendeka -tendana kwa vitenzi vya silabi moja haukubaliki. Pengine hali hii inatokana na tofauti kubwa iliyopo baina ya mofu hizi kwani utendeka hutokea baada ya kitenzi ilhali utendana hutokea kabla ya kitenzi.

### Mfuatano wa Mofu Nyambulishi za Utendana +Tendeka (//-kwi - + -isik-//)

Mfuatano wa mofu nyambulishi unaohusisha utendana – utendeka //-kwi- + -isik-// kwa vitenzi vya silabi moja haujitokezi katika lugha ya Kihehe. Watoa taarifa hawajathibisha ikiwa lugha yao ina mfuatano wa mofu. Vitenzi vyote vivyojaribiwa uwandani havikuonesha ruwaza hiyo. Vilevile, uchunguzi uliofanyika kwa njia ya mahojiano haujabaini kuwapo kwa mfuatano huo. Kutokana matokeo haya, tunashawishika kutoa dai kuwa mfuatano wa mofu nyambulishi unaohusisha mofu nyambulishi za utendana na tendeka katika vitenzi vya silabi moja haupo katika lugha ya Kihehe. Kama ilivyodokezwa hapo awali, kiisimu hali hii inaweza kuwa imesababishwa na tofauti za kimazingira ya utokeaji baina ya mofu hizo. Mofu // -kwi-// hutokea kabla ya mzizi wa kitenzi wakati mofu //-isik-// hutokea baada ya mzizi. Kutokana na nafasi zitokeazo mofu hizi mbili katika kitenzi cha lugha ya Kihehe, ni vigumu kupata mfatano wa *utendana na utendeka*.

### Mfuatano wa Mofu za Utendeka +Tendana (//-ik- + -kwi- / -an-//)

Data ya uwandani inaonesha kuwa mfuatano wa mofu nyambulishi wenye ruwaza zautendeka – tendana //-ik- + -kwi-/-an-// katika lugha ya Kihehe haukubaliki. Vitenzi vilivyojaribiwauwandani kwa njia ya hojaji na mahojiano havikudokeza kuwapo kwa mfuatano huo. Aidha, watoataarifa wazee wa umri kati ya 50-80, kadhalika hawakudhihirisha utokeaji wa mfuatano huo. Hivyo, ni dhahiri kwamba lugha hiyo haina ruwaza za mfuatano wa mofu nyambulishi baina ya mofu utendeka-utendana katika vitenzi vyenye silabi zaidi ya moja. Hali hii pia, inathibitishwa na maana zinazoibuliwa na vitenzi vinavyoelekea kukubali huo mfuatano. Kwamba, maana hizo ni za kiprag-

matiki pekee.

## Mfuatano wa Mofu za Utendana + Tendeka (//-kwi-/-an- + -ik-//)

Data iliyokusanywa na kuchanganuliwa kutoka uwandani inaonesha kuwa mfuatano wa mofu ya utendana na utendeka unaojitokeza ni ule unaohusisha mofu ya utendana //-an-// ambayo hunyambulishwa baada ya mzizi wa kitenzi tu. Hivyo, mofimu tendana (-an-) huungana na mofu tendeka (-ik-) na kuunda mnyambuliko wa utendana - utendeka //-an- + -ik-//. Data katika mfano wa 4 hapa chini unadhihirisha hali hiyo:

| 04. **Kihehe** | | | | **Kiswahili** |
|---|---|---|---|---|
| (a) lek- | an- | ik- | a | achanika |
| (b) long- | an- | ik- | a | semanika |
| (c) wung- | an- | ik- | a | unganika |
| (d) gav- | an- | ik- | a | gawanika |
| (e) wulag- | an- | ik- | a | uanika |

Mofimu: Mz + Tdn + Tdk + Ii

Mifano hiyo katika 4 hapo juu inaonesha kuwa mfuatano huu wa vitenzi unakubalika. Aidha, data hiyo inaonesha namna baadhi ya vitenzi vyenye silabi zaidi ya moja vikiwa na ruwaza ya mfuatano wa mofu nyambulishi ya utendana + utendeka //-an- + -ik-// hususani kwa umbo tendana //-an-// pekee. Hivyo, mfuatano wa mofu utendana - utendeka unakubalika katika vitenzi vyenye silabi zaidi ya moja. Utokeaji wa mfuatano huo unaweza kurasimishwa kikanuni kama katika 04:

04. //-an- + -ik-// ⟶ - an- +-ik- | Mz
a-
e-
-o-
u-

## Hitimisho

Makala haya yalilenga kubainisha mfuatano wa mofu nyambulishi za utendeka na utendana katika vitenzi vya lugha ya Kihehe. Kisha kuunda kanuni zinazoukilia mfuatano huo. Katika kufikia lengo hili, utafiti uliandaa hojaji na mahojiano kwa wazawa wa lugha ya Kihehe. Vitenzi vya lugha Kihehe viligawanyika katika kategoria mbili, vitenzi vya silabi moja na vitenzi vyenye silabi zaidi moja. Katika uchunguzi huu, imebainika kwamba, mfuatano wa mofu nyambulishi za utendeka nautendana kwa vitenzi vya silabi moja haupo kabisa katika Kihehe. Sababu unayoukilia kukosekana kwa mfano huo, kunasababisha na nafasi ambamo mofu tajwa hutokea katika kitenzi. Moja inatokeakabla ya mzizi wa kitenzi na nyingine inatokea baada ya mzizi wa kitenzi. Kadhalika, imebainika kwamba, mofu nyambulishi zinaelekea kujitokeza zaidi kabla ya mzizi wa kitenzi kuliko baada ya kitenzi. Makala yamehitimisha kwamba, mfuatano wa mofu nyambulishi za utendeka na utendana katika Kihehe siyo zalifu, kwa sababu hauruhusu maneno mengi kuundwa kutokana na mchakato huo. Ama, kwa upande wa vitenzi vyenye silabi moja, ni mfuatano mmoja pekee ndiyo unakubalika. Kanuni Akisi ya Baker (1985; 2002) imethibitishwa kwamba, unyambulishaji wa kimofolojia unaakisi unyambulishaji wa kisintaksia. Mabadiliko ya nafasi ya utokeaji wa mofu katika neno, imeathiri pia mpangilio wa muundo wa neno hilo katika sentensi. Hivyo, inapendekezwa utafiti mwingine ambao utakuwa mpana ufanyike ili kuongeza data na kupanua zaidi welewa juu ya mofu

nyambulishi ya utendana kuonekana inatokea kabla ya mzizi wa kitenzi. Upanuzi ujumuishesampuli ya watoa taarifa na hata idadi ya vitenzi vitakavyoshirikishwa.

## Marejeleo


Ashton E. O (1944). Swahili Grammar: Including Intonation, London, Longman Group Ltd.

Baker, M (1985). “The Mirror Principle and Morphosyntatic Explanation”. Katika: Linguistics Enquiry 16:373- 415.

Baker, M (2002). “Bulding and Merging, not Checking: the nonexistenceof (Aux)-SVO language” Linguistics Enquiry 33: 321- 328.

Doke, C. M (1943). Outline grammar of Bantu, Mimeographed and Johannesburg, University of the Witwatersrand.

Gawasike, A (2011). Mfuatano wa Mofimu Nyambulishi katika Vitenzi vya Kikinga. Tasinifu ya M.A. Kiswahili (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Gawasike, A (2012). Dhana ya Uambikaji katika Kiswahili. Katika Kioo cha Lugha. Juzuu (15), TUKI: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Guthrie, M (1948). The Classification of Bantu Language. London: Oxford University Press.

Jonsson, E (1949). [rev. 1954] Kinyang’wezi Grammatik. Tabora: Tanganyika, Svenska Pingstmissionen.

Kothari, C. R (2009). Research Methodology: Methods and Techniques, New Delhi, New Age Internation Publishers.

Manova, S na Mark, A (2010). “Modeling affix order in Affix Combinations1”, Special issues of Morphology, Manova, Aronoff (Wah.). DOL: 10.1007/S11525-010-9153-6.

Massamba, D. P. B (2016). Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B. (2011). Maendeleo katika Nadharia ya Fonolojia. Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M., na Hokororo, J. I (2012). Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na Vyuo. Dar es Salaam: TUKI.

Mcpherson, L (2008). A Descriptive and Theoretical Account of Luganda Verbal Morphology, Unpublished Bachelor Dissertation, Srips College.

Mgullu, R. S (1999). Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili, Nairobi, Long horn Publishers.

Mligo, E. S (2012). Jifunze Utafiti: Mwongozo Kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti yenye Mantiki, Dar es Salaam: EGYS.

Mtavangu, N. B (2008). “Tense and Aspect in Ikihehe”. Katika Occasional Papers in Linguistics, Dar es Salaam, Language of Tanzania Publications, Na. 3.

Mpalanzi, L (2010). An Analysis of tense and Aspect system in Ikihehe: A Case of affirmative and negative constructions. M.A. (Linguistics) Dissertation, University of Dar es Salaam.

Nurse, D (2008). Tense and Aspect in Bantu Languages. New York, Oxford University Press.

Schröder, H (2008). “Word Order in Toposa: An Aspect of Multiple Feature-Checking”. SIL, International and the University of Texas at Arlington. Publications in Linguistics 142.

Wesana-Chomi, E. (2017). Kitangulizi cha Muundo wa Viambajengo wa Sentensi za Kiswahili. Dar es Salaam: TUKI.